
JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MARIA MTAKATIFU, KIMARA



S.L.P. 55171, KIMARA

Claretian Missionaries

HISTORIA NA KUMBUKUMBU YA MIAKA 20
2003-2023



A. HISTORIA YA PAROKIA YA KIMARA, 2003-2023

Historia ya Parokia ya Maria Mtakatifu Kimara inaanzia mwaka 1984 ambapo Padre Recardo Osla, Paroko Msaidizi wa Parokia ya Ubungo-Msewe alinunua kiwanja kidogo Kimara Matangini ambapo Parokia ipo. Mwaka 1984-85 Padre Skacha Luciano, Paroko wa Parokia ya Ubungo - Msewe alijenga kituo cha maendeleo ya vijana na chekechea katika kiwanja hicho. Kituo kilikuwa kinatumika kama kituo cha sala na wakati huduma hizo zinaendelea kutolewa, waumini waliongezeka na Ibada za Jumapili zikaanza mwaka 1989 kikiwa bado ni kituo cha sala. Historia hii haiwezi kukamilika bila kuwatambua na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kwanza walioanzisha mchakato wa kuomba ibada kufanyika hapa Kimara mwaka 1989. Wajumbe hao ni: 1. Bi Sibilina Nsanya (ambaye bado yupo Kimara hadi sasa); 2. Bwana Benito Amri; 3. Bwana T. Romani; 4. Bwana Gervase Chillipweli na 5. Bibi Jane Mtenga

Viwanja viwili vya Kanisa Na. 29 na 31 vilipimwa mwaka 1990 pamoja na Eneo la Dini (Religious Site) Na 31 na kufikia hatua ya ramani kukubaliwa na kusainiwa na Mkurugenzi wa Upimaji wa Ramani tarehe 18/1/91.

Mwaka 1995 kituo kilipata hadhi ya Kigango chini ya Parokia ya Ubungo Msewe na somo wa Kigango alikuwa Bikira Maria Mama wa Mungu. Tarehe 30 Novemba, 2003 kigango kilipandishwa hadhi na kuwa Parokia ya Maria Mtakatifu Kimara.



Jengo la Kigango cha Kimara, 2002

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Shirika la Consolata na Paroko Piero Cravero wa Ubungo-Msewe kwa kuwapokea mapadre wa kwanza wa Kimara kwa wiki sita kabla ya kuhamia Kimara. Mapadre hao walitokea

shirika la Claretians Missionaries wakiongozwa na Padre John Francis. Tunatoa shukrani nyingi kwa Shirika la Claretian Missionaries kwa kukubali kuja kuendesha Parokia ya Kimara na kuleta Mapadre.

Ujenzi wa kanisa la Parokia ulianza mwaka 2004 na jengo jipya la kanisa la Parokia Kimara lilizinduliwa na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo mwezi Septemba 2006. Hadi sasa Parokia imezaa Parokia zingine tatu: *Parokia ya Mt. Maria Claret Michungwani (Mei 2016), Parokia ya Mt. Maria Magdalena Kimara Mtoni (Oktoba 2017) na Parokia ya Bikira Maria Msaada wa Daima Korogwe (2022)*.

B. DIRA:

Parokia ya Kimara kuwa jamii ya Waamini wenye imani thabiti, upendo, umoja, wachamungu na wenye kutenda haki kwa wote.

C. DHIMA:

Kujenga jamii inayotegemea na kumtanguliza Mungu, kuishi amri za kanisa, amri ya upendo, roho wa injili na kushiriki fumbo la Ukombozi

D. HUDUMA YA KIROHO

Parokia inatoa huduma za kiroho mbalimbali zikiwemo:

1) Misa Takatifu Jumapili
   a. Misa ya kwanza saa 12.00 asubuhi
   b. Misa ya pili saa 1.30 asubuhi
   c. Misa ya tatu saa 3.30 asubuhi
2) Misa siku za wiki: Jumatatu-Ijumaa Masifu Saa 12:00 na Misa takatifu saa 12.30 asubuhi,
3) Kuabudu Ekaristi Alhamisi saa 11.00 jioni
4) Kuabudu Ekaristi Ijumaa ya kwanza ya mwezi saa 11.00 jioni hadi saa 2.00 usiku
5) Misa Jumamosi ya kwanza ya mwezi saa: 12.00 asubuhi
6) Ibada Katika Jumuiya ama Somo wa Jumuiya/Kanda:

Kila Jumuiya/Kanda wanafanya ibada ya somo wa jumuiya /kanda mara moja kwa mwaka.

E. MASAKRAMENTI

Parokia imeendelea kutoa masakrament mbalimbali ambapo kuanzia mwaka 2003 hadi 2023 idadi ya waliopata sakramenti ni kama ifuatavyo:

1) *Waliobatizwa 6760*
2) *Waliopata Komunio ya Kwanza zaidi ya 5000.*
3) *Waliopata Kipaimara 4586*
4) *Waliofunga Ndoa 1251*
5) *Walipata Daraja la Upadre ni mmoja Padre Germin Laizer wa shirika la Camilians.*
6) *Walipata huduma ya Misa ya Mazishi 215*

Tangu kuanzishwa kwake, parokia imetoa masista watatu: kutoka Jumuiya ya Thomas Aquino, Jumuiya ya Mtakatifu Agape na Jumuiya ya Mtakatifu Antony wa Padua..

F. KAZI ZINGINE ZA KIROHO NA KUKUZA IMANI

Katika kuimarisha waamini kiroho, licha ya kutoa masakramenti mbalimbali, Parokia inao utaratibu wa kufanya mafungo, semina na hija kwa makundi ya vyama vya kitume na parokia kwa ujumla. Ratiba ya semina na hija ziko kwenye mpango kazi wa parokia wa kila mwaka. Aidha, Parokia imejenga kanisa dogo kwa ajili ya kuabudu ambapo waamini na makundi mbalimbali wanapata fursa ya kuabudu.

Huduma zingine za kiroho ni pamoja na Kubariki Nyumba – matembezi ya Ekaristi; kutembeza Msalaba kila Familia, Ibada mbali mbali za Misa – kwenye kanda, jumuiya na misa maalum. semina, makongamano na mafungo ya kiroho kikanda; Parokia imewahi kuratibu Hija mbali mbali Pugu, Bagamoyo, na Makanisa ya Hija DSM na nje ya nchi kama vile Namugongo Uganda, Nyakijogah, Kibeho Rwanda na Subukia Kenya.

G. VYAMA VYA KITUME

Parokia inasimamia na kulea vyama vya kitume katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa sasa Parokiani kuna vyama, mashirika na jumuiya za kitume 14: UWAKA, WAWATA, VIWAWA, Utoto Mtakatifu, UKWAKATA, Chama cha Moyo Mtakatifu wa Yesu, Legio Maria, Jumuiya za Neokatekuminato, Watumishi wa Altare, Karismatik Katoliki, Wajane na Wagane, Wazee na Wastaafu, Upendo group na St. Vincent wa Paulo. Parokia iko kwenye mpango wa kuanzisha vyama vya CPT na Utume wa Familia.

H. MATENDO YA UPENDO KWA PAROKIA DADA:

Parokia ya Kimara imeendelea kulea Parokia ya Kisiju Mkoani Pwani kwa kufanya matendo ya upendo kila baada ya miezi mitatu kwa kupeleka mahitaji kwa wahitaji na pesa za kuchangia huduma za Parokia. Pia Maparoko na wajumbe wa Kamati Tendaji hutembelea Kisiju kadiri nafasi inavyopatikana.

I. KUUNDA JUMUIYA NDOGO NDOGO.

Mwaka 1991 Jumuiya mbili ziliundwa nazo ni Blue Army na WAWATA. Kazi iliyokuwa ngumu na ya muhimu kwa wakati huo ilikuwa ufuatiliaji na upatikanaji wa hati miliki kwa viwanja vya Kanisa.

Kwa sasa (2023) Parokia ina kanda 9 na jumuiya 39 ambazo ni:

1. ***Familia Takatifu (Jeshini A)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Cesilia, Mt. Vicent wa Paulo, Mt. Katarina na Mt. Philomena
2. ***Bikira Maria Mkingiwa Dhambi Ya Asili (Jeshini (B))*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Laurent,Mt. Malaika Mikaeli, Mt. Joachim, na Mt. Maria Magdalena
3. ***Utatu Mtakatifu (Kanisani)*** Inaundwa na jumuiya za Familia Takatifu, Mt. Anthony Maria Claret, Mt. Elizabeth, Mt. Kizito na Mt. Polycarp
4. ***Mt. Merinje (Matangini)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Anselmo, Mt. Karoli Boromeo, Mt. Karoli Lwanga, na Mt. Zakaria

5. ***Mt. Petro (Stop Over A)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Anthony wa Misri, Mt. Malaika Rafael na Mt. Brigita
6. ***Mt. Paulo (Stop Over B)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Anna, Mt. Ritha wa Kashia, Mt. Yakobo Mtume, Mt. Fransisca wa Roma na Roho Mtakatifu
7. ***Mt. Mukasa (Tanesco A)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Dominico, Mt. Fransisco wa Asis, Mt. Fransisco wa Giloramo, Mt. Luka na Mt. Theresia wa Avila
8. ***Mt. Agustino (Tanesco B)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Agape, Mt. Fransisco wa Sale, Mt. Fransisco Xavery, Mt. Martin Depores na Mt. Paulino
9. ***Mt. Monica (Tanesco C)*** Inaundwa na jumuiya za Mt. Yohana Mbatizaji, Bikira Maria wa Rozari, Mt. Albert Mkuu na Mt. Yuda Thadei

Parokia ya Kimara inakadiriwa kuwa na waumini 4,500.

J. WATU MASHUHURI WA KUKUMBUKWA

Katika miaka ya uhai wa parokia tangu ilivyoanza kama kituo cha sala mwaka 1989, watu mbalimbali walijitoa zaidi kuifikisha Parokia hapa ilipo leo. Baadhi ya watu wa kukumbukwa:

1. Mwadhama Polycarp Cardinal Pengo aliyekuwa Askofu wa Jimbo kwa kutoa kibali cha kuwa Parokia.
2. Mapadre wa Seminari ya Segerea na Baraza la maaskofu waliokuwa wanakuja Kigangoni kusaidia kusoma misa pamoja na Padre Merchant aliyesoma misa ya kwanza Kimara, Padre Severini Niwemugizi, Padre Daminai Dalu, Padre Evaristo Chengula na Padre Liundi. Mapadre Severini Niwemugizi, Daminai Dalu na Evaristo Chengula kwa sasa ni maaskofu.
3. Bwana Gervas Chilipweli- Alisaidia upatikanaji wa Eneo la kwanza la kanisa na upatikanaji wa Mapadre wa kwanza kuja kuadhimisha misa Kimara wakati bado kituo na Kigango; Alikuwa Mwenyekiti wa Kwanza wa Kituo cha sala 1989-1995.
4. Bwana Anthony Kiyanga Mwenyekiti wa mwisho wa Kigango na wa kwanza wa Parokia (1995-2006) na pia mjumbe wa kamati ya ardhi

iliyoshiriki katika mchakato mgumu wa upatikanaji wa hati ya kiwanja cha Kanisa

5. Mama Sibilina Nsanya mwanamama pekee katika Halmashauri ya Walei ya Kwanza na pia aliyeshiriki kutafuta mapadre wa kwanza kabla haijawa Parokia
6. Bwana Protas Nyoni Makamu Mwenyekiti wa Kwanza wa Kigango (1989), Katekista wa pili hapa Kimara na Katekista wa kwanza baada ya kuwa Parokia, na Katekista aliyehudumia muda mrefu nafasi hiyo. Mzee Nyoni pia alikuwa mjumbe wa Kamati ya Ardhi aliyepambana kupatikana kiwanja cha kanisa na kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa hati ya Kiwanja cha kanisa akishirikiana na Bwana Ladislaus Salema.
7. Bwana Benito E. Amri- Katibu wa kwanza wa Kigango
8. Bwana Mathias Mkanwa- Katibu Msaidizi wa kwanza wa Kigango
9. Bwana Desderi Mchomvu-Mweka Hazina wa kwanza wa Kigango
10. Mama Clementina Nyoni- Mjumbe katika Halmashauri wa Walei ya Kwanza
11. Mama Sibilina Nsanya- Mjumbe Halmashauri wa Walei ya Kwanza
12. Bwana Anselm Assenga- Mjumbe Halmashauri wa Walei ya Kwanza
13. Bwana Rogasian Asenga- Mjumbe Halmashauri wa Walei ya Kwanza
14. Bwana Raphael Sengwila- mjumbe (Kwaya) Halmashauri wa Walei ya Kwanza
15. Anthony Sanga - mjumbe (Kwaya) Familia ya Alfred Sarungi kwa Kukarimu ugeni unapokuwa umetembelea nyakati hizo, na pia ndiyo walio uzia kanisa kiwanja cha kituo cha maendeleo bondeni.
16. Injinia Ladisilaus Salema Mwenyekiti Kamati Ujenzi wa Kanisa, yeye na familia ilitoa michango mikubwa mno kwenye ujenzi tutawakumbuka daima.
17. Bwana Otto Mosha kwa ushiriki wake katika ujenzi akiwa na Mzee Aselemo Asenga na Ndugu Albert Makyao. Mzee Otto Mosha alikuwa mfuatiliaji wa karibu wa viwanja na pia ndiye kiongozi aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi, katika ngazi mbalimbali kuanzia mwaka 1991

akiwa kama mweka hazina wa kamati tendaji ya kituo cha sala, na sasa (2023) ndiye mweneyekiti wa wazee na wastaafu Parokiani.

18. Bwana Reginard Mengi kwa mchango wa Paa la Kanisa
19. Bwana Thomas Lyimo kwa ujenzi wa Paa la Kanisa
20. Bwana John Mwanyika kwa kuhudumu muda mrefu katika kamati ya Litrujia ambaye alifundisha wanakamati wengi, Pia Mwanyika atakumbukwa kwa majitoleo yake kwa pamoja na hali yake ya kipato kuwa cha kawaida, lakini alitoa fremu mbili za biashara katika nyumba yake Kimara Korogwe ili zitumike kusaidia wahitaji, wakati huo Korogwe kilikuwa Kigango cha Kimara.
21. Bwana Stanslaus Nguma ambaye aliwahi kuwa mjumbe wa kamati tendaji, na kwa moyo wake wa ukarimu alitoa fremu tano za biashara katika nyumba yake Kimara Korogwe wakati huo ilikuwa ni sehemu ya parokia ya Kimara ili zitumike kusaidia wahitaji, wakati huo Korogwe kilikuwa sehemu ya Parokia ya Kimara .
22. Mrs Anne Salema, alijitoa kupamba Kanisa kwa miaka mingi. Mama Salema alikuwa mpambaji wenye kipaji kikubwa. Pia aliwahi kuwa menyekiti wa WAWATA.
23. Mrs Adela Macha aliyekuwa WAWATA ambaye aliupenda wito huo na alitumia karama hiyo kwa uaminifu kuimarasha WAWATA na pia alihudumu kama MC.
24. Bibi Magdalena Yeronimo kwa mchango wake mkubwa wa miaka mingi katika kuleta maua ya kupamba altare.
25. Injinia Kapistran Haule, Injinia Philip Mpemba na Bwana Madege kwa kazi kubwa ya ujenzi wa jengo la Kanisa
26. Mhashamu Baba Askofu Methodius Kilaini, Mheshimiwa Luteni Yusufu Makamba akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar e slaam wakati huo na Monsignor D. Mbiku kwa kuendesha Harambee mbili za Kwanza kuchangia ujenzi wa Kanisa.
27. Mr Charles Misango MC aliyehamashisha kwa kiwango cha juu harambee na michango ya ujenzi wa kanisa kwa kutumia kauli mbiu wa ‘HUKUNA KULALA’ na kuwezesha kanisa kujengwa kwa muda mfupi

28. Padre John Francis CMF aliyesimamia utafutaji fedha na ujenzi wa Kanisa
29. Padre Sahaya Raj CMF aliyesimamia utafutaji fedha na ujenzi wa nyumba ya mapadre na kanisa la kuabudia
30. Padre Jesuraj Michael CMF kwa kutafuta fedha na kununua kiwanja kikubwa kwa ajili ya kanisa jipya na miundombinu ya Korogwe
31. Padre Timothy Ogutu CMF kwa uthubutu uliowezesha kuanza ujenzi wa kituo cha maendeleo ambacho kikikamilika kitatumika kwa ufundi stadi na malezi ya vijana

K. MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITANO 2008-2012 NA 2020-2025

Parokia imetayarisha mpango mkakati wa miaka mitano mwaka 2008-2012 na mwaka 2020-2025. Pia kumekuwa na mipango ya utekelezaji ya mwaka mmoja mmoja, na ratiba ya kichungaji kwa kila mwaka.

L. UJENZI WA MIUNDOMBINU YA PAROKIA

Utekelezaji wa majukumu ya kiroho unategemea sana mafanikio katika ujenzi wa miundo mbinu. Parokia tangu izinduliwe kwa kupitia Kamati Tendaji imetekeleza ujenzi wa miundo mbinu ifuatayo:

1. Ununuzi wa Kiwanja cha kituo cha Mendeleo 2003
2. Ujenzi wa Kanisa Kimara 2004
3. Ununuzi wa Kiwanja cha zamani cha Korogwe 2005 palipojengwa kanisa la sasa la Korogwe
4. Nyumba ya mapadre 2013
5. Ununuzi na kiwanja cha Michungwani
6. Ununuzi wa Kiwanja cha Kimara Mtoni



Jengo la Kanisa 2004



Nyumba ya Mapdre 2013



Kanisa la Kuabudia 2016



Ukumbi wa Muda 2018

7. Ununuzi wa Nyumba ya Katekista,
8. Ujenzi wa Kanisa la kuabudia 2016
9. Kuanzisha ujenzi wa Kigango cha Kimara Mtoni 2017
10. Kuanzisha ujenzi wa kigango cha Michungwani 2018
11. Ujenzi wa fremu kwa ajili ya kuhudumia wahitaji,
12. Ujenzi wa Ukumbi wa muda bondeni 2018
13. Kuendesha mradi wa maturubai yanayotumika kwenye ibada za sikukuu watu wanapokuwa wengi.
14. UJenzi wa Ofisi ya walei 2019
15. Ujenzi wa Kanisa la muda la watoto 2019
16. Ujenzi wa Duka la visakramenti 2019
17. Ununuzi wa Kiwanja kipya kwa ajili ya Kanisa na Nyumba ya Mapadre Korogwe, 2022
18. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Maendeleo kitakachokuwa na ghorofa nne, 2022 unaotarajiwa kukamilika mwaka 2024.



Kituo cha Maendeleo, ujenzi umeanza 2022

M. MIRADI YA VYAMA NA VIKUNDI PAROKIANI

Aidha, kuna miradi ya ujasiriamali wa kuwajengea uwezo wa vyama kujiendesha: Utengenezaji wa vipeperushi siku za dominika; Utengenezaji wa mishumaa; Kikundi cha mapishi wanaotoa huduma kwenye hafla za parokia; Utengenezaji wa sabuni; Ukodishaji wa vyombo vya muziki kwa ajili ya sherehe za parokia na parokia jirani na makongamano ya kidini

N. CHANGAMOTO NA MKAKATI WA KUKABILIANA NAZO

Sehemu yeyote yenye mafanikio changamoto hazikosekani. Upande wa Kiroho, kuna changamoto ya ushiriki hafifu wa wanaume na vijana katika jumuiya na matukio ya kanisa. Uongozi wa kanisa wakati wote umekuwa

unatafuta mbinu za kukabiliana na changamoto hizi kwa kufanya uhamasishaji wa mara kwa mara, na hivi karibuni kumekuwa na ziara za kuwatembelea waumini kwenye jumuiya zao ili kuongea nao na kujadili namna ya kupunguza changamoto hizi.

Historia ya Kimara haijakamilika bila kutaja changamoto kubwa ya ardhi ambapo wananchi wamevamia ardhi ya kanisa kwa miaka zaidi ya ishirini, hata pale mahakama ilipotoa haki kwa kanisa bado utekelezaji wake unacheleweshwa. Parokia ilipata pigo lingine mwaka 2017 kwa jengo la kanisa kubomolewa na TANROADS. Pamoja na kanisa linamiliki kiwanja cha kanisa kihalali kuanzia miaka ya tisini na kupata hati miliki halali mwaka 2009, bado mamlaka za serikali ziliendelea na zoezi la ubomoaji. Ubomoaji huu umesababisha kanisa kupungua ukubwa na hivyo kushindwa kupokea waamini wengi kwa mara moja, na kuna shida kubwa ya maegesho. Kanisa limeendelea kudai haki yake kupitia vyombo vya sheria na wakati tunasubiri ufumbuzi kanisa limetafuta maeneo mbadala ili kuendelea na utume wa kuinjilisha na huduma kwa jamii.

o. **VIONGOZI WA KIROHO**

Tangu kuzinduliwa kwake, shughuli za kiroho zimeendelea kutolewa na mapadre wa shirika la Mt. Maria Claret (Claretian Missionaries, CMF), ambapo kumekuwa na maparoko wanne hadi sasa (Fr. Francis - miaka 7; 2003-2010. Fr. Sahayaraj - miaka 8; 2010-2018, Fr. Jesuraj Michael Miaka 3; April 2018- April 2021) na Fr. Timothy Ogutu (April 2021 hadi sasa).

Aidha kumekuwapo na Maparoko Wasaidizi 12 hadi sasa (Fr. Sahayaraj Michael (CMF) 2003-2005, Fr. Jesuraj Michael (CMF) 2005-2006, Fr. Christu Raj(CMF) 2006-2007, Fr. Peter Rwezahura 2008-2009, Fr. Martin Amalanathan (CMF)2009-2010, Fr. Emmanuel Vedamuthu (CMF) 2010-2012. Fr. Wolfgang Michael Tengia (CMF)2012-2013, Fr. Gido Nikolaus Shayo (CMF) 2013-2015, Fr. Anyanwu Chukwuemeka (CMF)2015-2017, Fr. Allan Kibidi N'goga (CMF) 2017-2019, Fr. Alfred Tukamushaba (CMF)February 2020- April 2021) na Fr. Vicent Ojwang (2021 hadi sasa)

Parokia ilipata masista wa kwanza wanne kutoka Shirika la Masista wa Benedictine wa Mt.Agnes. Chipole, Songea tarehe 24/8/2004, nao walikuwa:

Sr. Antonia Kapinga OSB - Sista wa Nyumba; Sr. Hekima Kayombo OSB- Katekista; Sr. Bakhita Nchimbi OSB– Huduma za Kanisani; na Sr. Rehema Mbunga OSB – Mwalimu wa Chekechea. Baadae Sr. Rehema Mbunga OSB aliondoka akamuachia Sr. Mbarikiwa Tawete OSB , baadae akaja Sr. Sponsor Chis kama karani wa Parokia ambaye naye alimuachia Sr. Upendo naye akamuachia Sr. Gracia Lyamukuyu kama Karani wa Parokia. Alipohama Sr. Rehema Mbunga OSB aliingia Sr. Asumpta Ngonyani OSB kama Katekista na kwa ajili ya watoto ambaye alimuachia Sr. Shangilio OSB ambaye naye alimuachia Sister Shangilio OSB aliyemuachia Sr Sophia Mbeya OSB ambaye yupo hadi sasa (2023). Sr Glory Lwena wa Sakristia alimpokea Sr Bhakita mwaka 2010 na yupo hasa sasa 2023 na hivyo kuwa sista aliyehudumu miaka 12, muda mrefu kuliko masista wengine waliotoa huduma Kimara.

Pamoja na Masista wa Benedictine wa Mt .Agnes Chipole, Songea wanaotoa huduma Parokiani, pia ndani ya Parokia kuna mashirika mengine mawili ya Masista, shirika la Daughters of Mary Immaculate (DMI) na Masista wa shirika la Mt. Charles Borromeo.

Tangu kuzinduliwa kama Parokia wafuatao wamehudumu hapa Kimara: Katekista Protas Nyoni; Katekista Gido Msisi; Katekista Gloria Luckly Malisa; Katekista Sr. Heckima Kayombo OSB, Katekista Sister Shangilio OSB, Katekista Valentine Nyandoga, Katekista David Mwaleni na Katekista Joyce Njaku. Kwa sasa yupo Katekista Valentine akishirikiana na Sister Sophia Mbeya OSB.

'Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele'. ***Zab 23:6***

MAWASILIANO YA PAROKIA:
S.L.P. 55171, SIMU+255 745 079438
parokiakimara2003@gmail.com

